

USANIFU WA LUGHA KATIKA UANDISHI WA EBRAHIM HUSSEIN

Geoffrey K. King'ei

Katika fasihi ya kimaandishi ya Kiswahili, utanzu wa tamthilia kama ule wa riwaya ni wa hivi karibuni na hauna tarehe ndefu au ukwasi mwingi wa maandishi kama utanzu wa ushairi. Lakini hivi si kusema kuwa Waswahili au Waafrika kwa jumla hawakuwa na taaluma ya maigizo au sarakasi kabla ya majilio ya sanaa za maandishi za kimagharibi kama vile riwaya, tamthilia sinema na kadhalika.

Miongoni mwa watunzi maarufu wa tamthilia za Kiswahili yumo Ebrahim Hussein. Mtunzi huyu amejipambua kama mwanasanaa mwenye kipawa kikubwa cha kusarifu fikira na mawazo mazito na kuyawasilisha kisanaa katika umbo la tamthilia. Kwa hakika haitoshi tu mtu kuwa na kipawa. Uwezo wowote au ujuzi aliojaliwa nao mtu pia huhitaji kupaliliwa na kunolewa kila mara kupitia majaribio na mazoezi. Kama wasemavyo Waingereza, mazoezi huleta matokeo fika yaliyokamilika; nao Waswahili wamesisitiza kwamba "kinolewacho kupata". Tunapoyachunguza maandishi ya E. Hussein tangu tamthilia ya Alikiona 1970, Wakati Ukuta 1970 hadi Arusi (1980) tutaona namna mwandishi huyu alivyokua na kustawi kisanaa. Kazi zake zote ambazo tutazirejelea katika makala haya zinaonyesha ushahidi wa maendeleo katika vipengele vya lugha, fani na maudhui.

Kwa minajili ya makala haya nitachunguza kwa ujumla jinsi E. Hussein alivyomudu matumizi ya lugha kama mbinu au chombo cha kusafirishia ujumbe wake katika tamthilia zake. Kutokana na lengo langu, haiyamkiniki katika makala ya aina hii kujadili kwa tafsili kila lililo muhimu kuhusu hoja ya mjadala. Kwa sababu hii nitapitia tu kwa jumla baadhi ya mbinu za lugha na usanifu kwa jumla alizozitumia E. Hussein katika uandishi wake. Shabaha yangu sio hasa kuchambua kwa undani kinadharia lugha ya mwandishi bali kutoa ufafanuzi ambao unaweza kutuungazia zaidi katika juhudi zetu za kuyaelewa maandishi ya E. Hussein. Katika kujadili matumizi ya lugha nitagusiagusia hapa na pale kuhusu hoja au maudhui yanayowasilishwa ili kutoa ufafanuzi ufaao.

Tamthilia za kwanza mbili za E. Hussein zilichapishwa pamoja kama kijitabu kimoja kinachoitwa Michezo ya Kuigiza (1970). Tamthilia hizi ni Alikiona na Wakati Ukuta. mnariri

wa kijitabu hiki ameusifia uwezo wa mwandishi wa kuimiliki vilivyo lugha ya Kiswahili. Katika jalada amesema,

"Katika michezo hii Ebrahim amesaidia kuinua lugha ya Kiswahili katika daraja mpya, akiitumia kwa ustadi na imani ya kipawa alichojaliwa wa magudulia anavyochezea udongo mikononi mwake kuleta sura aina kwa aina."

Katika Alikiona, E.Hussein anaeleza hasara na utovu wa uaminifu kati ya walicoana. Katika usimulizi wake wa vituko na mtiririko wa visa vyenyewe, mwandishi amejaribu kutumia lugha nyepesi na sentensi fupi fupi. Katika maandishi yake yote, Hussein anaonyesha wazi kuwa anapendelea kutumia mazungumzo na majibizano mafupi mafupi. Mtindo huu unashabihiana sana na ule wa kishairi. Kwa hakika baadhi ya matumizi yana athari ya lugha ya kishairi. Kwa mfano Saida na Abdalla wanapongea, Abdalla anamwuliza Saida.

"Unasema kwa dhati au kwa chati,"¹

Vile vile Omari anaposhindwa na vipingamizi vya mkewe Saida anamwambia,

"Lahaula wee!
Nikikataa vita
Nikikubali ngondo. Sasa nifanye nini?
Hebu niambie mke wangu, nifanye nini au niseme nini?"²

Naye Mama Pili anamjibu Omari anapomwuliza habari kwake atokako kwamba,

"Hivyo hivyo tu hakuchi, kunakucha"³

Matumizi ya lugha kama hii ya kishairi hayapatikani kwa wingi katika tamthilia ya Kinjeketile. Pengine hii ni kwa sababu Kinjeketile ni tamthilia iliyotungwa kwa maandishi ya kinathari ili kurahisisha yale masimulizi wala lengo lake si kutilia mkazo fikira na mawazo kadha kwa kutumia lugha kama katika Mashetani, Arusi na Jogoo kijijini.

Tukiangalia kwa mfano katika Mashetani kutoka ukurasa wa kwanza tunaona lugha anayoitumia shetani mhusika mara nyingi imefuata muundo na mtindo wa lugha ya kishairi. Lugha hii ina ulinganifu wa kimatamshi, marudio, msisitizo na mdundo maalumu. Kwa mfano shetani anasema,

"Unanijua mimi nani?
 Mimi shetani.
 Siyo jini wala kuhani.
 Mimi shetani.
 Uwezo wangu. hanifadhiki.
 Wema wangu hauhisabiki.
 Ubaya wangu hausemeki.
 Ninajenga.
 Ninabomoa.
 Ninatukuza.
 Ninadhalilisha nitakavyo.
 Mimi ni nguvu na nguvu ni mimi.
 Mimi ni uwezo na uwezo ni mimi⁴.

Hali kadhalika wimbo wa Binadamu katika onyesho hili ni shairi lenye mvuto japo halikutungwa kwa kuzingatia arudhi kikamilifu.

Anaimba hivi:-

"Wako wapi walio wakijitapa?
 Sasa twawataka.
 Wako wapi walio wakijitapa?
 Sasa twawataka.
 Tumekwisha (anacheka) wakamata
 Wakamata
 Tumekwisha wabwatabwata.
 Wako wapi waliokuwa juu jana?
 Sasa twawataka.
 Wako wapi waliokuwa juu jana?
 Sasa twawataka.
 Tumekwisha waangusha
 Waangusha.
 Tumekwisha wasagasaga
 Tumekwisha wakamata
 Wakamata
 Tumekwisha wabwatabwata
 Tumekwisha waangusha
 Waangusha.
 Tumekwisha wasagasaga."⁵

Mtindo huu wa kishairi ulifikia kilele chake cha ufanisi katika hadithi au ngano za E. Hussein zilizochapishwa mnamo 1976 kwa jina Jogoo kijijini na Ngao ya Jadi. Kama mchapishaji na mhariri walivyoeleza, katika tungo hizi mpya Ebrahim Hussein amechanganya mbinu za masimulizi ya mapokezi ya fasihi simulizi kama ngano na vitendawili pamoja na ufundi wa fasihi andishi ambao ameutumia kutungia hadithi hizi kwa muundo wa maigizo jukwaani.

Ngano hizi mbili ni mfano maridhawa wa jinsi fasihi simulizi ilivyo na ukwasi wa miundo na fani mbalimbali.

Kwa kufuatisha mbinu za masimulizi ya kimapokezi ngano hizi zinaanza kama ngano za kiasili kwa maamkuzi na majibu na baadaye ufunguzi. Majibizano ni kati ya msimulizi (mtambaji hadithi) na wasikilizaji wake (kiitikio).

"MTAMBAJI HADITHI: Paukwa
KIITIKIO: Pakawa
MTAMBAJI HADITHI: Paukwa
KIITIKIO: Pakawa
MTAMBAJI HADITHI: Hapokale, palikuwa na mkunazi
KIITIKIO: Naam twaiib
MTAMBAJI HADITHI: Mkunazi Mkubwa pita kiasi"⁶

Sasa masimulizi yanaendelea hadi pale unapokaribia mwisho wa kisa chenyewe ndipo mtambaji hadithi anapomalizia masimulizi yake kwa kusema,

"Basi hapa kaditamati
Kadi tamati kalimati
Maneno yamenisaliti
Na kisa pia kimenikaukia
KIITIKIO:
Kisa tumekisikia
Utungo' metuelea
Maneno' metuingia
Ama maana hatujaambulia
MTAMBAJI HADITHI:
Basi nipeni mji
KIITIKIO:
Nenda Kigoma
MTAMBAJI HADITHI:
Hapana asilani
KIITIKIO:
Nenda Dodoma
MTAMBAJI HADITHI:
Hapana asilani
KIITIKIO:
Nenda Dar es Salaama
MTAMBAJI HADITHI:
Sasa maana tawatolea"⁷

Kutokana na madondoo hayo mawili yaliyopo hapo juu, tunaona kwamba mtindo huu wa uandishi licha ya kutumia majibizano, pia unatumia ushairi na mbinu nyinginezo za matu-

mizi ya lugha kama vile marudio na 'ufupishaji wa maneno. Mbinu ya marudio ni muhimu sana katika masimulizi kutilia hoja fulani mkazo na pia kuleta athari fulani katika masikizi. Licha ya hayo marudio humwezesha msikilizaji (au msomaji) kujenga picha au taswira iliyo makini na bayana juu ya yale anayoelezwa. Kwa mfano, msimulizi anapoeleza jinsi kijana aliyejitolea kafara alivyoanguka chini na kutulia kwa masikitiko ya dhambi za kijiji, anasema kwa kurudia,

"Muda si muda
Lahaula kajikwaa
Lahaula kajikwaa
Kajikwaa kateleza
Kateleza kaanguka
Kaangukia kitovu cha ardhi njema
(Kituo)
Mkono huku
Mkono kule
Mguu huku⁸
Mguu kule"

Kwa jumla tunaweza kusema kwamba Hussein amejaribu kufuata sio tu mtindo wa masimulizi ya ngano bali pia wa tenzi za kiafrika. Utenzi mara nyingi huwa na urari wa vina vya mwishoni mwa kila msitari na pia msitari wa kipokeo au kina cha kipokeo huwa a au ma. Aghalabu tenzi nyingi za kiafrika na hasa za Kiswahili zina mazungumzo na pia masimulizi katika nafsi ya pili au ya tatu na zote huwa zina mtindo wa "ufunguzi" na "kimalizio". Kama zilivyo tenzi zote, ngano hizi za E. Hussein zimetungwa kusimulia maisha na vitendo vya kishujaa vya viongozi na jamii fulani katika juhudi zao za kupigana na dhuluma na matatizo mengine ya kijamii.

Ebrahim Hussein amejitahidi sana kutimiza mlingano wa vina vya mwisho vya misitari yote na kupata kina cha kipokeo cha a katika ngano hizi bila kupoteza maana yake na bila kubandika vina visivyoleta muumano wa kimaana. Kwa mfano ile njia waliyojia walowezi na baadaye kutoweka imeelezwa kishairi hivi:-

"Ikaacha alama zake
Ikaacha athari zake
Ikaacha kwaruzo zake
Kila mahali ilipojipitia
Na ingawa manyunyu yalinyesha
Ingawa mito ilijifurisha
Na bahari ilijitutumsha⁹
Lakini alama hazikufifia"

Ingawa hivyo aina ya ushairi alioutumia E. Hussein katika Arusi(1980) ni tofauti na ule mtindo wa utenzi upatikanao katika Jogoo kijijini na Ngao ya Jadi(1975). Humu katika Arusi mna mazungumzo mafupi mafupi kwa kila mhusika ambayo hayana ulinganifu wa vina hata kidogo. Lakini ingawa hivyo mazungumzo haya yana mpingo na mtiririko wa kishairi. Kwa mfano Ali anamwambia Kahinja hivi,

"Naipenda fikira
Iliyoojaa
Pana kama bahari;
Nikiogelea,
Au nikipaa
Mwishowe si dhahiri,
Fikira nyembamba
Huhadaa
Huwa tasi la akili,
Na utu
Mahali duni huuweka"¹⁰

Mtiririko na muundo wa maneno haya ni wa kishairi na ni tofauti kabisa na ule wa mazungumzo ya Somo anapomshauri Mwanaheri kabla ya kuolewa katika onyesho la nne(uk.10-11). Lakini isitoshe hata hayo mazungumzo ya somo yana mdundo dhahiri wa kishairi. Kwa mfano anaposema:-

"Kaa somo yangu. Maana we ni somo yangu. Ingawaje usomo wenyewe ule mara nyingine unapenda kuutatanisha. We umesikia kwa nani? Siku kama leo kwenda kuirahisisha? Na watu wengine duniani kote siku hii bei huipandisha? We kwenda kuonana na mumeo leo kabla ya arusi. Si kujifedhehesha?"¹¹

Ni wazi kuwa E. Hussein huwapa wahusika wake aina ya lugha inayolingana na hadhi na tajriba ya kila mmoja. Kwa mfano katika Arusi, Somo na Shangazi ni watu wazima na lugha yao ni ya kiutu uzima yenye staha na adabu. Pose, Ali na Lily ni vijana nao huzungumza kama wafanyavyo vijana wengine. Bukini na Bwana Mzuri nao ni makabaila ambao hawana wakati mwingi wa kuzungumza na makabwela. Ingawa Kahinja ni kijana, Hussein amemteua kuwa chombo chake cha kuelezea falsafa na fikira za mwandishi. Falfasa hii tutaipitia baadaye. Naye Mwimbaji kwa vile ni msanii, anafinyanga lugha yake ya nyimbo kishairi. Anaimba hivi kuhusu kusalitika kimapenzi:

"Kivuli kama mwaka;
Kimya kimya kama paka
Maisha linyemelea.

Na Mola alipoweka
Rangi zochangamka
Kivuli kilijipitia.

Mwana akanyweeka,
Ingawa kicheko kilimtaka
Lakini huzuni ilimkumbatia.

Akapinda huku akipenda
Kila miaka ilivyowanda
Ye alizidi kujikondea"12

Sasa tugeukie upande mwingine wa uandishi wa E. Hussein nao ni matumizi yake ya taswira na jazanda. Licha ya kutumia lugha yenye maana fiche sana, Hussein ameonyesha ustadi mkubwa katika kubuni na kuchora jazanda zenye undani mkubwa zinazotuwezesha kuelewa zaidi yale anayotusimulia. Katika fasihi jazanda zinaweza kuchukua miundo au sura kadha na vile vile zinaweza kuwa na sifa tofauti. Kwa mfano jazanda inaweza kuwa ni msemu tu wa maneno maalumu yenye maana ya undani au hadithi au chombo kilichopewa sifa au maana isiyo ya kawaida. Hakuna sheria za kumwongoza mtu katika kusarifu jazanda au taswira fulani muradi mtu yule aonyeshe ulinganifu uliopo baina ya maneno ayatumiayo na maana anayoikusudia. Kadhalika hapana mwongozo wowote katika kufasiri maana ya jazanda. Fasiri kama ile huwa ni kama vile kufasiri ndoto. Uhakika wa ile fasiri hutegemea uhusiano uliopo baina ya maana ya ndoto na jinsi ilivyofasiriwa kumaanisha. Katika fasihi, fasiri sahihi ya jazanda hutegemea ujuzi wa anayefasiri juu ya mtunzi na jamii yake pamoja na maudhui ya masimulizi.

Jazanda lazima ijengwe kutokana na msingi wa ulinganifu baina ya dhana, jambo au chombo kinachorejelewa na jazanda ile iliyochorwa. Kwa msingi huo jazanda au taswira hueleza ukweli wa ulinganifu huo kimaisha. Kwa mfano matumizi ya Hussein ya maneno na dhana kama "wakati Ukuta", "Manyoya", "Shetani", "Chewa", "Mashua", "Binadamu", "Ngazi", "Jogoo", "Ngao", "Arusi", "Mbuyu", "Kisu" na kadhalika ni ya kijazanda na yote yanaeleza maana na misimamo ya mwandishi kuhusu siasa, uchumi na historia ya jamii yake. Haja ya mwandishi atumiapo jazanda au taswira sio kuwakanganya wasomaji wake kama wengi wetu tunavyofikiri bali ni kueleza maana kwa undani na kwa njia ya kisanaa. Jazanda zinapotumiwa ipasavyo katika fasihi huimarisha maana na kuyapamba maandishi yake ili yaeleweke vyema zaidi na kuyapa nguvu na uhai mpya.

Tukianza na tamthilia ya Wakati Ukuta, tutaona kwamba kile kichwa chenyewe ni jazanda ambayo imetokana na msemu

maarufu wa Kiswahili, "Wakati Ukuta, ukipigana nao utaumiza mkono wako." Wazazi wa Tatu hawatambui mapito ya wakati yamezaa mabadiliko makubwa ya kijamii. Pia katika upande mwingine Tatu na Swai nao hawatambui kuwa uhuru wanaojitakia una mipaka na majukumu yake. Wameshindwa kutambua kuwa mategemeo na uhusiano wao na wazazi wao hauwezi kuondolewa na mabadiliko ya wakati.

Katika tamthilia ya Arusi, Hussein ametumia mila za Waswahili kuhusu arusi ili kueleza kimafumbo ukweli fulani kuhusu siasa za nchi yake. Kwanza kabisa neno "arusi" limepewa maana maradufu. Kuna arusi ya Mwanaheri na Bukini na pia kuna "arusi" ya kimawazo, ambayo inampitia Mwanaheri katika akili yake tu. Arusi hii ya kimawazo inaelezea uhusiano uliopo baina ya mataifa yenye mifumo na itikadi tofauti za kisiasa na kiuchumi. Kwa upande mmoja tunao mfumo wa kijamaa unaowakilishwa na Mwanaheri na kwa kiasi fulani Kahinja. Kwa upande wa pili tunao mfumo wa kibepari wa kimagharibi unaowakilishwa na Bukini na Bwana Mzuri na kiasi fulani umewaathiri wafu kama Ali, Rose na Lily. Kutofaulu kwa ile ndoa basi ni dhihirisho la kutosha kuwa nchi zenye mitazamo tofauti ya kisiasa haziwezi kushirikiana vizuri bila ya nchi moja kuinyonya au kuinyanyasa nyingine.

Bila shaka ni katika tamthilia ya Mashetani ambamo E. Hussein ametumia jazanda na taswira kwa wingi zaidi kuliko katika tamthilia nyingine yoyote yake. Kichwa chenyewe "Mashetani" ni jazanda yenye maana nyingi kama alivyolitumia neno lenyewe. Kama asemavyo Kitaru, shetani ana maana nyingi sana na huja kwa njia nyingi vile vile:-

"Shetani, hii ni nafsi yenye ncha nyingi, ni kiumbe kinachomwingia binadamu kwa namna mbalimbali na kumzunga akili. Shetani hufahamu? Hadithi chungu nzima juu ya shetani na binadamu zinazoeleza vipi shetani anavyomjia binadamu na kumghilibu kwa sura mbalimbali"13.

Neno "Shetani" limetumiwa kwa maana ya 'pepo wabaya' ambao wanaweza kumpagaa mtu hadi pale pepo wale watakapopungwa. Hii ndiyo maana aliyonayo mamake Kitaru. Yeye anafikiri Kitaru na Juma wameingiliwa na mashetani pale mbuyuni wanapocheza. Pia kulingana na Mfaume, shetani huwa ni kiini au chanzo cha maovu au dhambi zote anazozifanya mtu kwa udhaifu wake. Yeye huona bora kumsingizia shetani kuliko kukiri lawama kwa vitendo vyake. Mfano mzuri ni yule dereva ambaye

aliangusha gari na kumsingizia shetani kwa kudai "shetani, kazi ya shetani," kama anavyohadithia Mfaume.

Lakini maana aliyo nayo Kitaru ni tofauti na ni ya kisiasa. Kulingana na maelezo ya Kitaru, "shetani anaweza kuwa rafiki yako, baba yako, ndugu yako --- ". Maana hii inatueleza kuwa shetani hapa limetumiwa kuelezea tabia fulani. Katika tamthilia hii kwa mfano tabaka la Kitaru ni la 'mashe-tani" yaani mabwanyenye na manaizi waliomiliki mali na vyeo vya mabepari wa kikoloni waliong'olewa baada ya uhuru. Mitindo yao ya maisha ni ya kikabaila. Kwani wao ni wanyonyaji na lengo lao kubwa ni kulimbikiza mali ya umma. Mfano mwingine wa 'shetani' ni mhusika Mtu 1 na vile vile yule mwenye gari anayepita mbele ya mkahawa. Tunaelezwa lile gari amelinunua kwa kuifisidi kampuni ya umma hadi ikafilisika.

Maana ya mwisho ya neno shetani tuliyopewa katika Mashetani ni ya 'shetani' ambaye ni mkoloni mtawala. Katika sehemu ya kwanza ya tamthilia hii tunamwona 'shetani' akimha-ngaisha 'Binadamu' kwa kumwamrisha na kumtesa kwa kila njia. Katika utangulizi huu wa tamthilia, twaonyeshwa vile mkoloni kwa udhalimu na uchoyo alivyotukandamiza sisi kwa utawala wake wa kimabavu na kikatili. Kwa ujanja wake, mkoloni anapohisi hana budi kumpa mtawaliwa uhuru wake, anamfundisha mtawaliwa lugha na utamaduni wake ili masilahi yake yeye mkoloni yazidi kuhifadhika. Sifa alizopewa shetani ni ujanja, ukatili, kiburi, uwongo, uzuzu, mijitutumuo na vitisho.

Kuna jazanda na taswira nyingi nyingine katika tamthilia hii ambazo hatuwezi kuziacha katika fasiri yetu ya tamthilia ya Mashetani. Baadhi ya Jazanda hizi tunaweza kuziorodhesha na kuzifufunua kwa maneno machache.

1. UKWELI uk. 12, uk. 56-57

Ukweli umetajwa kama suluhisho la mgogoro unaosaba-bishwa na tofauti za kisiasa na kiuchumi. Neno hili linamaa-nisha chanzo au asili ya tofauti hizi.

2. MCHEZO

Neno hili linamaanisha maisha ya kila siku, maingiliano ya watu wa matabaka na hali tofauti katika kazi na maisha ya kawaida.

"Ikiwa yote yalianza katika mchezo huu ambao ni kitendo, basi jawabu iko katika mchezo huu huu. Tukiucheza na kuucheza na kuucheza, mwisho wake itatoka sumu yake"14

Maneno niliyoyapigia msitari pia yana umuhimu wake. Kwa ufupi Hussein anatumia kuwa mgogoro wa kisiasa na kijamii ulizalika kutokana na kitendo cha kihistoria ambacho kinaweza kumaanisha hapa kujinyakulia uhuru, mapinduzi ya Zanzibar ya January 1964 au kupitishwa kwa Azimio la Arusha la mwaka wa 1967.

'Vitendo' vyote hivi viliacha athari kubwa sana za kisiasa kwani vilimaanisha kupanda ngazi au 'kushuka ngazi' kwa matabaka mbalimbali ya Watanzania. 'Sumu' hapa ni zile fikira au kumbukumbu za chuki na wivu walizokuwa nazo wale walioshuka ngazi kama familia ya Juma. Fikira kama zile zitakwisha tu iwapo matabaka haya tofauti yangekubali kuishi ('kucheza') pamoja na kusahau tofauti zao.

3. KISU (uk. 8-9)

"Kisu" kinamaanisha uwezo, juhudi au maarifa ambayo Waafrika waliotawaliwa na wakoloni walijipatia na ambayo yaliwawezesha kupigania uhuru wao na kumng'oa mkoloni.

4. CHEWA (uk. 28)

Katika hadithi waliyosimuliwa na bibi yake Juma, Chewa ni kiumbe mkubwa aishiye baharini na ambaye ana nguvu za kumeza kila kitu humo baharini. Anaweza kuilazimisha mashua iende isikotaka kwa kuvuta mkondo wa maji. Mfano huu tunaweza kuulinganisha na ule wa "mfalme Jeta" katika Kusadikika¹⁵. Neno chewa limetumiwa kimajazi kuonyesha ulafi na nguvu za mkoloni hasa katika mfumo wa ukoloni - mamboleo. Nchi changa huru huwa mara nyingi hazina hiari ya kujiamulia mambo yao mpaka mkoloni aje awaonyeshe "mapito yafaayo" na ambayo yeye atafaidika kiuchumi. Mataifa haya hushindwa kuepuka au kujitanzua na mnaso huu wa ukoloni mamboleo kama vile rubani wa chombo kama mashua ashindwavyo kukielekeza njia ambayo abiria wake (raia) wangependa kwenda.

5. JAHAZI (uk. 21)

Huu ni mfano wa kuendeleza dhana ya ukoloni mamboleo. Nchi changa za Kiafrika zilizojinyakulia uhuru wa bendera huwa ni kama mfano wa Jahazi ambalo abiria na nahodha hawana hiari ya kujiamulia njia watakayopita. Wakoloni kwa kutumia mbinu za ukoloni mamboleo za kisiasa na kiuchumi huweza kuyamiliki tena mataifa hayo. Viongozi na raia wa mataifa hayo hulazimika kuzingatia kitumwa mapenzi ya mkoloni. Mkondo wa maji baharini ndio unaolivuta jahazi upande uendako

na nahodha hawezi kupingana na mkondo. Hali kadhalika mkoloni ana masilahi yake ambayo si lazima mara nyingi yafanane na yale ya mataifa machanga kwa hivyo mataifa yanatumikia tena mkoloni bila kujua jinsi ya kujiepusha na mara nyingi bila njia ya kujiepushia. Swala kubwa ni je, uhuru una maana gani iwapo viongozi na raia wa nchi huru bado wanabakia vyombo vya kumtumikia mkoloni aliyewatawala?

6. MBUYU (uk. 1)

Mbuyu miongoni mwa jamii nyingi za Kiafrika ni mti mtakatifu na mara nyingi uliachiwa kukua na kuwa mahali patakatifu pa kutolea kafara. Madhabahu yalijengwa pale chini ya ule mti hasa penye miamba na mapango ambapo sadaka za wanyama na binadamu na pia maombi na mashauri mbalimbali baina ya watu na mizimu yao yalifanyiwa.

Katika Mashetani, mchezo unaanza na kuishia kwenye pango lenye mbuyu mkubwa. Katika imani na itikadi za kidini, madhabahu si mahali pa kutisha bali ni mahali pa pekee pa usalama. Ni mahali ambapo watu walikwenda kutafuta suluhisho, mwongozo au maagizo ya miungu wao kutokana na matatizo yao. Katika tamthilia hii, tatizo ambalo vijana hawa wawili yaani Juma na Kitaru wamekwenda kulisuluhisha pale pangoni ni kuhusu tofauti kati ya familia zao hasa kufuatia mapinduzi ya mwaka wa 1964. Mapinduzi haya yalisababisha kushuka kwa akina Juma katika ngazi za kisiasa na kiuchumi na pia kupanda ngazi hizo kwa akina Kitaru. Tofauti hizi zilizua kutoelewana, chuki, dharau na shauku baina ya pande zote mbili. Basi hapo palizuka haja ya watu wote wale kuelewa siasa na historia ya nchi zao ambazo ndizo zilizozaa mapinduzi na kusababisha tofauti kati yao. Elimu hii ndiyo vijana wale waliyoiendea kule pangoni. Hivi ndivyo anavyoamaanisha Binadamu anaposema

"Ukweli lazima utafutwe.
Lazima nisafiri, safari ndefu
Nikajitafute, nikajisake
ili nijue mimi nani? Ili nijue
maana ya kitendo changu"16.

Lakini kwa watu waovu kama wezi, wahalifu na wachawi madhebehu huwa ni mahali pa kutisha na kuogofya na panapositahili kuchukiwa. Hii ndiyo sababu mama Kitaru anahofia kule kwenda kwa Kitaru na Juma kule pangoni. Maneno haya anayoyasema yametumiwa na Mwandishi ili kutueleza kwa kinaya kuwa wazazi wa Kitaru hasa mama yake ndiyo vile vile wanaozidisha dhiki ya Kitaru

kwani wao hawamsaidii kuelewa uhusiano wake .na Juma.
Mama yake kwa unafiki anasingizia 'mashetani' wa pangoni

"Namuogopea Kitaru. Mimi nafikiri
kakumbwa na shetani maana hawa
wanakwenda kucheza mbuyuni,
ule mkubwa. Na mimi ninajua ule
mbuyu mbaya. Una hatari kweli kweli."17

Tumeeleza matumizi ya lugha katika Mashetani kwa urefu kidogo kwa sababu tamthilia hii ndiyo iliyozusha mjadala juu ya muundo, lugha na maudhui yake kuliko kazi yoyote nyingine ya Ebrahim Hussein. Kwa jumla tunaweza kusema kuwa Hussein amedhihirisha bayana katika uandishi wake kuwa yeye huthamini sana fikira nzito nzito za kifalsafa kuliko kutegemea sana vitendo vya mchezo katika jukwaa. Aghalabu lugha ya E. Hussein ni lugha yenye maana fiche katika maandishi yake yote. Si rahisi kupata sehemu yoyote katika maandishi yake yenye mawazo yatiririkayo moja kwa moja yenye maana wazi na ya juu juu. Kila mojawapo ya tamthilia zake ina tasnifu zote hizi zimefinyangwa kwa mawazo mwafaka ya kifalsafa na kuzielewa msomaji hana budi kujizamisha katika akili ya mwandishi mwenyewe ili kuifasiri tasnifu ipasavyo.

Tumeona katika Kinjeketile, Kitunda anapozidi kumkera Kinjeketile ili aamru vita vianze, Kinjeketile anafikiri sana na kumweleza Kitunda kimafumbo kuwa

"Ntu huzaa neno, na neno likawa kubwa
kuliko ntu"18

Hii inamaanisha kuwa uamzi wa Kihistoria kama ule wa kumpiga mkoloni, huweza kuwa na matokeo makubwa. Kama nilivyotaja Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi ni ngano zilizoundwa kutokana hadithi halisi za mapokeo ya Kiswahili. Kwa mhasari kisa cha Jogoo Kijijini kinasimulia kuja kwa kundi la walowezi waliopasua njia ndefu baharini. Walipofika pale kijijini hawakukawia kuwateka wenyeji wao na kukiharibu kila walichokikuta mle kijijini.

Wala wakati mwingi haukupita
Miti ya Kitongoji tukaikata
Na mafundi wao tukawakamata
Mlango wetu Mkuu kutuumbilia."19

Majilio haya yalizorotesha nchi nzima kwa kila

hali. Badala ya mahaba, huruma na ihsani iliyotawala nyoyo za wenyeji kabla ya wageni hao waovu kuja kijijini kutokana na matunda ya ule mti ulioitwa "mkunazi - Rahmani", sasa mioyo yao na 'utu' wao ukatoweka. Ndwele iliyoiua mkunazi na kuleta ugonjwa huu wa chuki na ukatili iliambukizwa na walowezi waliokuja kijijini.

Wageni walipokuja hawakuelewa wenyeji walivyo - hasirika na jinsi walivyokuwa wamewaandaa "mchwa shababi" wa kuihami nchi yao. Baadaye "mchwa janabi" walisababi-sha kung'olewa kwa mizizi ya walowezi na kuufanya 'utu katika rutuba ukajiotea". Lakini walowezi hawakuelewa bado yote yaliyokuwa yakitendeka kwani "sikio (lao) lilikuwa sikio la kufa." Ilibidi kufanywe kafara kubwa ili kufidia hasara iliyoletwa na kule kukaribishwa kwa wale walowezi waharibifu waliokifisidi kijiji. Kafara hii ilitokana na kujitolea kwa kijana mmoja mzuri ambaye alijitwisha 'dhambi' za kijiji kizima ili kukikomboa.

"kijana kuusikia ukweli
Hata hakuhuzunika asili
Mabega yake wasaa wawili
Yalibeba madhambi ya ile njia"²⁰.

Lakini ingawa walowezi waliondoka kijijini na kurudi makwao waliacha athari kubwa sana ambazo hazikuwa rahisi kuziondoa. Tunaelezwa kuwa njia yao walowezi iliacha athari.

"Ikaacha alama zake
Ikaacha athari zake
Ikaacha kwaruzo zake
Kila mahali ilipojipitia"²¹.

Kisa hiki cha Jogoo Kijijini kimesokoteka kweli kimaudhui na kimuundo. Lugha ya fumbo lenyewe inakifanya kisa chenyewe kigumu kueleweka.

Hadithi ya Ngao ya Jadi ni rahisi kidogo kuifahamu kwa kuwa mtiririko wake ni mwepesi na vitushi vyake vimeungika vizuri kuliko katika Jogoo Kijijini. Hapa katika Ngao ya Jadi tunaelezwa kuja kwa Joka kubwa lililoitwa sesota lenye vichwa sabini. Joka hili linaanza kuhangaisha wanakijiji kwa kuchukua mali na binti zao kila siku. Iliwabidi wanakijiji wakamkabidhi mtemi wao 'Ngao ya Jadi' iliyowekwa na Tewa na pia ule 'Mkuki wa tangu Hawa' aliouweka Mkwawa, wakampa mtemi ili aende kulisaka lile Joka na kuliulia mbali. Mtemi

analisaka na kuliua Joka. Hapo ikawa ni furaha na vigelegele kushangilia kifo cha Joka lile fisadi.

"Hapo katoka yowe
Na vingi vigelegele
Nd'o kina dada wale
'Lipiga wapigavyo
Azaliwapo mtoto dume mmoya"²².

Lakini baada ya muda kidogo nchi ikaingia najisi ya ufisadi wa kila aina. Wenyeji walianza kumwiiga mgeni Joka aliyeuiliwa na wengine hasa wa jamii ya Mtemi wakajitwalia mali za nchi na kuzitumia wao binafsi. Basi yakazuka matabaka hasa tabaka la wale waliochukua uongozi baada ya Joka kung'olewa. Hili ni tabaka la kina Pambo. Tunaelezwa,

"Na sisi 'kina Pambo
Tukaja zusha mambo
Tukafanya urembo
Magamba ya Joka tukajivalia
Na rafiki wa Mtemi
Wakawa stadi wa uchumi
Bi Mwema kamtia mbaroni
Yasmini
mikononi mwao kajifirigisha"²³

Matokeo ya hali hii yalikuwa ni kutokeza tena kwa Joka sesota pengine katika hali nyingine. Tunaelezwa kuwa,

"Wale watu wal'ojua
Ishara 'kaitambua
Yakini wakaijuwa
Sesota kichwa cha pili
awaletea"²⁴

Basi ni dhahiri kuwa kisa hiki cha pili si kigumu sana kukifasiri tukizingatia hali za siasa, historia na uchumi katika nchi ya Jamhuri ya Tanzania, anayosi-mulia E. Hussein. Isitoshe hali inayosimuliwa kwa mfano wa ngano hizi za kuvutia imo katika mataifa mengi machanga.

Jambo kubwa kuhusu lugha ya kifalsafa katika tamthilia ya Arusi ni kule kutofautishwa kwa mifumo miwili ya kisiasa; mfumo wa kijamaa na ule wa kibepari. Tumekwisha dokeza hapo juu kuhusu maana ya 'Arusi' na

pia jinsi wahusika wa kimajazi walivyotumiwa katika tamthilia hii ili kufafanua ujumbe wa mwandishi. Mhusika Kahinja ndiye mwanafalsafa na mara nyingi katika uzungumzaji wake yeye anaeleza fikira na maoni ya mwandishi kuhusu mifumo ile miwili ya kisiasa. Hatosheki na mfumo wa ujamaa wa nyumbani kwao Tanzania, na anaeleza kuwa mtu hana budi kuelewa mifumo mingine ya siasa katika mataifa ya kigeni ili kupanua ujuzi na mtazamo wake wa kimaisha. Anasema -

"Nimetoka sipendi kukaliana,
Napenda nafasi, wasaa
Wasaa mwingi sana
Na sipendi kuongelea juu ya mambo ya nyumbani
kwa sababu sipendi
kuongelea habari ya ndoa".²⁵

Kahinja anavuka mpaka na kuingia Kenya katika mji wa Mombasa. Baada ya kujifunza juu ya mfumo wa Kenya wa siasa anaamua kuendelea na safari yake ya kimawazo ili kutafakari zaidi juu ya siasa za nchi zote mbili.

"Sasa Mombasa
Haiwezi tena kuninasa
Natafuta pembe ya kujiendea.

Nami kwangu ukimya
Katika wangu mtima
Kazi huenda ukajifanyia"²⁶

Kila mfumo una uzuri na udhaifu wake na hapana siasa moja yenye kukamilika hasa pale mipaka ya utu na uadilifu inapokiukwa. Siasa yoyote ifaayo sharti ijengwe katika "chimbuko la asili" yaani historia na utamaduni halisi wa taifa lenyewe. Mfumo wowote wa falsafa ya siasa hauwezi kuwafaidi watu wa kawaida au raia iwapo unapuuza masilahi ya umma au ya mtu binafsi. Katika siasa ifaayo ubinafsi lazima uepukwe na kulaaniwa. Kahinja anasema,

"katika nusu kuna ulazimifu
Na kutaka mzima huwa njozi ya ukamilifu
Katika mzima kuna upungufu
Na kutaka nyingi huwa njozi ya isirafu
Na huu ndio ugonjwa naoukimbia"²⁷.

Kahinja amegundua kutokana na utafiti wake kuwa itikadi yoyote ya kisiasa inayomviza mtu kimawazo kwa

kutompa uhuru wa kibinafsi na kimawazo huwa ni falsafa isiyofaa na huwa ni sawa na utumwa. Anatuambia.

"Naipenda fikira
Iliyojaa
Pana kama bahari
Nikiogelea
Au nikipaa,
Mwishowe si dhahiri,
Fikira nyembamba
Huhadaa,
Huwa tasi la akili
Na utu
Mahali duni huweka."²⁸

Uongozi usio na dhamira ya kuendeleza watu wake ni mbaya uwe ni wa kijamaa au kibepari. Hauna tofauti yoyote kama asemavyo Hussein kupitia mhusika Kahinja,

"Sitaonja
Raha au furaha ya kujifikia
Ikiwa ni hivyo
Nje au ndani.
Tofauti sitajionea"²⁹

Kutokana na ujumbe uliomo katika tamthilia hii ya Arusi ni wazi kuwa E. Hussein anaamini katika kutekelezwa kwa masilahi ya jamii nzima na pia ya watu binafsi katika jamii hiyo. Hii ni kwa sababu kutokana na tajriba ya Kahinja tunaona kuwa mfumo wa kijamaa unajishughulisha sana na masilahi ya jamii na kusahau au kupuuza watu binafsi katika jamii. Huu ni udhaifu. Vile vile nao ubepari unathamini sana mahitaji ya mtu binafsi hivi kwamba ubinafsi unatawala na kuhatarisha masurufu ya umma wote.

Kwa kumalizia tunaweza kusema matumizi ya lugha katika maandishi ya E. Hussein yanaonyesha uwezo wake wa kuisimua akili na hisia zetu kupitia chombo hiki cha lugha. Kwake yeye sanaa ndio uhai wa mawasiliano katika fasihi. Ametumia kunga nyingi katika mawasiliano yake na wasomaji wa tamthilia zake kama vile mtafaruku wa kimawazo, ukinzani, uzungumzi nafsia, ucheshi, hotuba na lugha yakinifu. Kwa mfano ili kutofautisha wahusika wake kisanaa kwa mujibu wa elimu, ujuzi, umri na mwelekeo wa kimawazo, Hussein amewapa wahusika wake mitindo ya lugha na lafudhi zinazowafikiana nao barabara. Mifano mizuri ni lugha ya wahusika kama vile Kitaru, Juma, Wazazi wa Kitaru, Swai na Tatu, Kahinja na Ali, Kitunda na Kinjeketile.

Ni jambo lisiloweza kupingwa kwamba ni wasomaji na wachambuzi wachache wayaonayo maandishi ya Ebrahim Hussein rahisi kueleweka. Pengine hili ni kwa kuwa E. Hussein kama baadhi ya waandishi wengine huthamini sana sana katika fasihi kuliko wepesi wa kupitisha ujumbe uliomo.

TANBIHI

1. Hussein E Michezo ya Kuigiza, EAPH, Nairobi, 1970 uk. 45.
2. Kama hapa juu uk. 49.
3. " " " " 52
4. E. Hussein, Mashetani, OUP, Dar es Salaam, 1971, uk. 1
5. Kama hapa juu uk. 9-10.
6. Hussein E., Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi OUP, Dar es Salaam, 1976, uk. 13.
7. Kama hapa juu uk. 31-32
8. " " " " 18
9. " " " " 27
10. Hussein E. Arusi, OUP, Dar es Salaam, 1980, uk. 9.
11. Kama hapa juu uk. 10-11.
12. " " " " 3.
13. Mashetani uk. 24-25
14. " " " 56.
15. Robert S. Kusadikika, Nelson, 1971; uk. 25-26
16. Mashetani uk. 12
17. " uk. 27
18. Hussein E. Kinjeketile, OUP, Dar es Salaam, 1969, uk. 28.
19. Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi, uk. 25.
20. Kama hapa juu uk. 28
21. " " " " 27
22. " " " " 44
23. " " " " 47
24. " " " " 48
25. Arusi uk. 18
26. Kama hapa juu uk. 20
27. " " " " 8
28. " " " " 9
29. " " " " 40